Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: +255 22 2773038/48, Fax: +255 22 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz,
Website www.humanrightstz.org.tz

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

UVAMIZI NA KUKAMATWA KWA WAANGALIZI, VIFAA BINAFSI NA VIFAA VYA KITUO CHA UANGALIZI WA UCHAGUZI MKUU 2015

TAREHE: 31 OCKTOBA 2015

Ndugu wanahabari,

Mtandao wa Asasi za Kiraia za Uangalizi wa Chaguzi - TACCEO/ Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu - LHRC katika zoezi la kukamilisha uangalizi wa uchaguzi mkuu wa Ocktoba 2015, siku ya Alhamis Tarehe 29 Ocktoba 2015, mnamo majira ya saa nane mchana tulivamiwa na kikosi cha Jeshi la Polisi waliokuwa na gari aina ya defenda iliyojaa Polisi walio kuwa na mavazi ya kujihami, kofia za chuma, bunduki na fimbo. Pamoja na Polisi walio vaa sare za Polisi na wengine sita waliokuwa wamevalia mavazi ya kiraia.

Polisi hao sita waliovaa mavazi ya kiraia na mmoja aliyevaa vazi la jeshi la Polisi waliingia katika ofisi za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Mbezi na kudai kuwa walikuwa wameagizwa na waliyoiita ***'Mamlaka ya Juu'*** kuja kukamata waangalizi na vifaa vya kieletroniki vilivyokuwa vinatumika katika zoezi zima la uangalizi wa uchaguzi. Polisi hao waliongozwa na mkuu wa upelelezi Wilaya ya Kipolisi Kawe, **ASP Mgonja** na baadae msaidizi wa kamanda wa Polisi mkoa wa Dar es Salaam **ndugu Salum**. Polisi walieleza maafisa waangalizi wa uchaguzi kuwa wamepata taarifa kuwa kituo kina kusanya na kusambaza taarifa za uchaguzi zisizo rasmi. Katika zoezi hilo Polisi walikusanya na kukamata komputa za mezani

24, komputa mpakato 3, simu 25 za ofisi na simu binafsi za waangalizi na kuwakamata waangalizi wetu 36.

Waangalizi na vifaa hivyo vilichukuliwa na kukabidhiwa Kituo Kikuu cha Polisi cha Kati (*Central*) na baadae kupelekwa Makao makuu ya Polisi. Baadhi ya Waangalizi walichukuliwa maelezo siku ya tarehe 29 usiku na wote 36 walidhaminiwa na kutakiwa kurudi Polisi tarehe 30 Oktoba 2015 kukamilisha zoezi la kutoa maelezo kwenye shitaka chini ya kifungu namba 16 cha Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya mwaka 2015, ambacho kinasema kwa kingereza:

"*Any person who publishes information or data presented in a picture, text, symbol or any other form in a computer system knowing that such information or data is false, deceptive, misleading or inaccurate and with intent to defame, threaten, abuse, insult or otherwise deceive or misleading to the public or counseling commission an offence, commits an offence and shall on conviction be liable to a fine not less than five million shillings or to imprisonment for a term not less than three years or to both".*

Tafsiri ya Kiswahili isiyo Rasmi ni;

"Mtu yeyote ambaye atachapisha taarifa, au data iliyotolewa katika picha, maandishi, ishara au aina yoyote katika mfumo wa kompyuta akijua kuwa taarifa hiyo au data ni uongo, danganyifu, yakupotosha au isiyo sahihi kwa lengo la kushusha hadhi , kutisha, kudhalisha, kutukana, kulaghai au ya kupotosha kwa umma anatenda kosa,na atakapobainika atatozwa faini ya shilingi zisizopungua million tano au kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu au vyote."

Baada ya zoezi la kuchukua taarifa kukamilika Waangalizi wetu 36, wanatakiwa kuripoti tena Polisi siku ya jumatatu Tarehe 2 Novemba 2015 kwa taratibu nyingine za kipolisi.

Ndugu wanahabari,

Sisi wana Mtandao wa Asasi za Kiraia - TACCEO tunalaani vikali uvamizi wa kituo chetu cha Uangalizi wa Uchaguzi kilichopo kwenye Sekretariati yetu ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kukamatwa kwa vifaa vyetu vya kielektoniki vya uangalizi wa uchaguzi (komputa na simu za mkononi), waangalizi wetu wa uchaguzi 36 na kukamatwa kwa simu zao binafsi na kunyanyaswa.

Suala hilo limejitokeza huku vyombo vya Serikali na vya Dola vikifahamu fika kuwa uangalizi huu wa uchaguzi ulifuata misingi iliyowekwa kikatiba na kuzingatia taratibu zote za kisheria.

Ndugu wanahabari,

TACCEO/ LHRC inaona uvamizi huu, kukamatwa kwa waangalizi wake 36 na vifaa vya uangalizi;

1. Unalengo la kudhoofisha ustawi wa demokrasia nchini, kupelekea kuwatisha wananchi kuweza kushiriki kikamilifu katika mambo yanayohusu mchakato wa chaguzi nchini na uwajibikaji wa Taasisi za serikali.
2. Unaondoa dhana nzima ya ushiriki kikamilifu wa sekta ya Umma na Binafsi *(Public Private Partnership (PPP))* katika kutoa maoni ya kuboresha demokrasia na Uchaguzi.
3. Pia uingiliwaji wa nafasi ya AZAKI kushiriki kikamilifu katika uangalizi wa chaguzi hapa nchini.
4. Kimejenga taswira kuwa wako watu au vyombo vilivyo juu ya sheria na kufuata taratibu za kutambulika kama mwangalizi kisheria haina maana katika mchakato wa uchaguzi nchini kama waangalizi na vifaa vyao vinaweza kukamatwa na wakazuiwa kukamilisha zoezi la uangalizi; na kwamba mamlaka yoyote kwa wakati wowote inavyojisikia inaweza kusimamisha zoezi la uangalizi ilhali liko katika taratibu za kisheria

Katika zoezi hili la kuvamiwa na kukamatwa kwa waangalizi na vifaa vya uangalizi wa Uchaguzi TACCEO/ LHRC umeathiri zoezi la uangalizi wa uchaguzi kwa viwango tofauti;

1. Kushindwa kukusanya taarifa za mwisho za uangalizi wa Uchaguzi kuhusiana na mapokeo ya matokeo ya uchaguzi kutoka kwa wananchi na wadau mbali mbali.

2. Kushindwa kukamilisha zoezi la ukusanyaji wa taarifa kutoka kwa waangalizi katika mikoa mbali mbali na kukamisha zoezi la uangalizi kama lilivyopangwa na kwa wakati.
3. Limegarimu muda wa waangalizi wa uchaguzi na rasilimali watu na rasilimali fedha mfano;
    i. Vifaa vikirudishwa vitahitaji kuunganilishwa upya kwenye mfumo wa TEHAMA wa kukusanya taarifa, kuwa na uwezekano wa kuharibu au kupoteza taarifa za uangalizi kitendo kitakachoathiri kazi ya uangalizi iliyoanza toka mwezi Aprili Mwaka huu (miezi 6).
    ii. Kuongeza muda wa kuendelea kuwa na waangalizi mpaka taratibu za kiPolisi zitakapokamilika kitendo ambacho kitaigarimu shirika,
    iii. Utoaji wa taarifa ya uangalizi wa uchaguzi ya awali baada ya Uchaguzi kukamilika.
    iv. Kuathiri utekelezaji wa kazi za siku hadi siku za TACCEO/LHRC

Kutokana na hayo TACCEO/LHRC inavitaka vyombo ya Dola na Serikali kama ifuatavyo;

1. Polisi

Jeshi la Polisi kufanya kazi zake kwa weledi na kuzingatia sheria na taratibu za kiutendaji za Polisi bila kupendelea wala kukiuka sheria kama ilivyofanyika kwa tukio hili, kuchukua hatua stahiki na za wakati kushughulikia suala hili ukizingatia kuwa kazi za uangalizi wa uchaguzi ni endelevu na zinahitajika kukamilishwa kwa wakati na muda stahiki.

2. Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Tunaitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi kututhibitishaa uhalali na uwepo wa nafasi, haki na wigo wa uangalizi wa uchaguzi nchini.

3. Serikali

Tunaitaka serikali na vyombo vyake kutokuminya nafasi za Azaki, waangalizi wa Uchaguzi na kuwa wazi katika taratibu na michakato ya kidemokrasia na chaguzi nchini.

Hitimisho

TACCEO/ LHRC inatoa wito kwa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kulaani kitendo hiki cha kukamata waangalizi na vifaa vya uangalizi wa uchaguzi nchini, kilichofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania kuwa ni kitendo chenye kuzuia ukuaji na kuminya ushiriki huru na wa haki wa wadau mbalimbali ikiwemo waangalizi wa uchaguzi chini ya asasi za kiraia nchini.

Imetolewa Kwenu na

Mtandao wa Asasi za Kiraia za Uangalizi wa Chaguzi (TACCEO)

Martina Kabisama

Mwenyekiti –TACCEO

UTARATIBU WA MTANDAO WA ASASI ZA KIRAIA ZA UANGALIZI WA CHAGUZI (TACCEO) KUANGALIA CHAGUZI NCHINI

Mtandao wa Asasi za Kiraia za Uangalizi wa Uchaguzi - TACCEO ni mtandao huru wa asasi zisizo za kiserikali, usiofungamana na chama chochote cha siasa wala kuendesha shuguli zake kwa minajili ya kujipatia faida, ulioanzishwa kwa madhumuni ya kuangalia mwenendo wa chaguzi kwa mujibu wa Sheria na Taratibu za Uchaguzi nchini.

TACCEO ni muungano wa asasi za Kiraia 17 zisizo za kiserikali ambazo zimesajiliwa kisheria na kufanya kazi zake Tanzania nzima ambazo ni; Legal and Human Rights Centre -LHRC, Tanzania Gender Networking Program - TGNP, Women Legal Aid Centre - WLAC, Southern African Human Rights NGO Network, Tanzania Chapter - SAHRINGON (Tanzania), Tanzania Media Women Association - TAMWA, ForDIA, Lawyers Environmental Action Team - LEAT, Policy Forum, Tanzania Legal Aid Network - TANLAP, Mwanza Policy Initiative - MPI, ACCORD, Tanzania Human Rights Forum -TAHURIFO, TLF, Youth Partnership Countrywide - YPC, HAKIMADINI, Zanzibar Legal Service Centre - ZLSC na Women in Law and Development - WiLDAF (Tanzania). TACCEO imekuwa na utaratibu na kufanya uangalizi wa chaguzi nchini kuanzia mwaka 2010, chaguzi ndogo za Igunga, Arumeru Mashariki, Kalenga na Chalinze. Pia TACCEO imeangalia uchaguzi wa Serekali za Mitaa mwaka 2014 na Uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2015.

Mtandao wa Asasi za Kiraia za Uwangalizi wa Uchaguzi (TACCEO) unaratibiwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni Shirika lisilo la Kiserikali liloanzishwa Mwaka 1995 chini ya Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 ya Sheria za Tanzania na imepata hati ya utambulisho kama Asasi isiyo ya Kiserekali chini ya sheria ya Asasi za Kiraia ya mwaka 2002. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaratibu michakato ya uangalizi wa Uchaguzi chini ya TACCEO.

KIINI CHA UANGALIZI WA UCHAGUZI

Malengo ya TACCEO ya uangalizi wa chaguzi ni kufanya tathmini ya viwango ambavyo michakato ya chaguzi ina heshimu misingi iliyoainishwa ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria na viwango vya Kikanda na Kimataifa vinavyohusu chaguzi. Hivyo huangalia mchakato mzima wa uandikishaji wa wapiga kura, michakato ya uteuzi wa wagombea ndani ya vyama, kampeni, taratibu zote za siku ya kupiga kura, kuhesabu, kujumuisha, kutangaza matokeo na mapokeo ya wadau mbalimbali kuhusiana na matokeo ya uchaguzi. Pamoja na hayo huangalia haki, fursa na ushiriki wa wananchi wote na makundi mbali katika mchakato mzima wa uchaguzi. Taratibu hizi zinasaidia kuboresha michakato ya uchaguzi na kukuza misingi ya demokrasia nchini.

UANGALIZI WA CHAGUZI KWA KUTUMIA TEHAMA

TACCEO/LHRC kwa mara ya kwanza mwaka 2010, ilifanya zoezi la uangalizi wa uchaguzi kwa kutumia TEHAMA. Pia utaratibu huu uliendelea kutumika katika uchaguzi wa serekali za mitaa mwaka 2014. Ambapo waangalizi wa uchaguzi walitumia simu za mkononi katika kutuma taarifa, ambazo zilipokelewa na kuthibitishwa kwenye kituo maalumu ambapo taarifa hizo baada ya kuthibitishwa ziliwasilishwa kwa wadau mahusi kulingana na taarifa iliyotolewa mfano; Jeshi la Polisi, Maafisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Takukuru na Wasimamizi wa Uchaguzi katika ngazi mbalimbali kwa ajili ya ufuatiliaji wa haraka pale ambapo kasoro zilijitokeza. Lengo kuu likiwa ni kusaidia utatuzi wa changamoto zilizoonekana katika mchakato wa uchaguzi ili kuhakikisha kuwa uchaguzi unaheshimu katiba na sheria za nchi. Baada ya kukamilika kwa uchaguzi, TACCEO/ LHRC huandaa ripoti ya majumuisho ya taarifa ya mchakato mzima wa uchaguzi na kuwakilisha ripoti kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na wadau mbali mbali.

UHALALI WA TACCEO/LHRC KUANGALIA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2015

LHRC mwaka huu wa 2015, kama ilivyokuwa kwenye chaguzi zilizopita iliomba kibali cha kuwa mwangalizi wa ndani wa uchaguzi mkuu kutoka kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa Sheria. Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia uchaguzi nchini. Hivyo LHRC ilipata kibali cha kuwa mwangalizi wa ndani kuangalia zoezi la

uandikishaji wa wapiga kura katika daftari la kudumu kwa mfumo wa kielektroniki wa BVR kwa barua kutoka Tume yenye **Kumb. Na. BA. 71/75/01/16** ambapo TACCEO/ LHRC ilituma waangalizi wake kila mkoa ambako zoezi hilo lilipokua linafanyika tangu lilipoanza **Tarehe 24 Februari 2015** hadi pale lilipokamilika **Tarehe 12 Septemba 2015**.

Ilikuendelea kufuatiwa uangalizi wa zoezi lililobaki la mchakato wa uchaguzi mkuu, LHRC iliandika barua ya kuomba uangalizi wa ndani na kutimiza vigezo vyote vilivyotakiwa na Tume. Mnamo **Tarehe 1 Septemba 2015,** Tume ya Taifa ya Uchaguzi baada ya kupitia na kujiridhisha kwamba LHRC imekidhi vigezo vyote vinavyohitajika ilikubali ombi na hivyo kuruhusu LHRC kuwa waangalizi wa ndani wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 kupitia barua yake yenye **kumb. Na. BA.74/75/01**.

Baada ya kupata kibali TACCEO/ LHRC ilishiriki kikamilifu katika zoezi la uangalizi wa uchaguzi kuanzia zoezi la uteuzi wa wagombea ndani wa vyama vya siasa kwa wagombea wa nafasi za urais, kampeni hadi wakati wa upigaji kura na utangazaji wa matokeo. TACCEO/ LHRC kulingana na Taratibu za Tume ilipata idhini ya Tume kwa waangalizi wake wote wa uchaguzi mmoja mmoja na iliweza kuwa na waangalizii 200 katika majimbo ambao waliangalia zoezi la kampeni mbali mbali katika majimbo, waangalizi wa muda mfupi 2100 ambao kazi yao kubwa ilikua ni kuangalia zoezi la upigaji kura, kuhesabu, kujumuisha matokeo na utangazaji wa matokeo kwa siku tatu yaani kuanzia siku moja kabla ya upigaji wa kura, siku ya kupiga kura na siku moja baada ya kupiga kura.

Kama ilivyokuwa awali katika uangalizi wa chaguzi mifumo ya TEHAMA ilitumika katika uangalizi wa uchaguzi Mkuu wa 2015. Hawa waangalizi wote tajwa hapo juu walikua wakituma taarifa hizo kwa njia ya mfumo maalumu wa mtandao. TACCEO/ LHRC walipokea taarifa hizo, kuthibitisha na kulingana na taarifa husika kutoa taarifa kwa vyombo husika ilikuchukuliwa hatua stahiki pale ilipobidi. Pia TACCEO/ LHRC kulingana na taarifa zilizokuwa zinakusanywa iliweza kutoa taarifa kwa umma kwa vipindi tofauti tofauti. Pamoja na hayo TACCEO/ LHRC inatarajia kutoa ripoti ya jumla ya uangalizi wa mchakato mzima wa uchaguzi mkuu 2015 na kuiwalilisha kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na wadau mbali mbali wa ajili ya kuboresha michakato ya chaguzi nchini.